



سیاہ فام غلام (Swahili)

Mtumwa Mweusi



Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS

Attar Qadiri Razavi

مستشرق
المعاصر

سِيَّاه فام غُلام

Siyah Form Ghulam



MTUMWA MWEUSI



Kitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi داعية بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wasiliana na Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu	ii
----------------------------------	----

MTUMWA MWEUSI 1

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ	1
Mtumwa mweusi.....	2
2. Uso wenye kung'ara.....	5
3. Mwanga wa mwenye nuru.....	5
4. Kuta kung'ara	6
5. Sindano iliyopotea	6
Vipi kuukanusha ubinadamu wa Mtume ﷺ?	7
6. Alimpa kumbukumbu nzuri.....	8
Kuwa na kawaida ya kusikiliza maongezi yanayotoa muamsho kuhusu sunna	9
Vipi nilijiokoa na upotofu!	10
7. Habari ya ghaibu	11
8. Ngamia wa ajabu.....	13
9. Simba wamefika	15
10. Wazazi wamefufuka.....	16

Wazazi wake walimpwekesha Allah عَزَّوَجَلَّ	17
Samaki aliemmeza Nabii Yunus عَلَيْهِ السَّلَام ni samaki wa peponi	17
Wazazi waheshimiwa wataingia peponi	18
11. Mbuzi aliekufa alihuika.....	18
12. Mtoto anafufuka.....	20
Aliemtusi mtume ametupwa nje ya kaburi.....	22
Kukanusha elimu ya mtume kumesababisha kifo kibaya....	24
Lulu za madani 14 kuhusu kupeana mikono	25
Kumuona Mtume Mtukufu ﷺ.....	27
Nilikuwa mpenzi wa filam za kigeni.....	28
Upendo kwa wacha mungu kunaleta thawabu ikiwa.....	29
Fadhila 8 za kupenda kwa ajili Ya Allah عَزَّوَجَلَّ	31

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ط

MTUMWA MWEUSI*

Vyovyote vile shetani atakavyo kufanya ujisikie uvivu, basi kisome kitabu hichi chote, utakuwa furahani *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ*.



Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ

Mtume wetu mpendwa aliebarikiwa amesema, 'Jibril *عَلَيْهِ السَّلَامُ* ameniambia kwamba Allah *عَزَّ وَجَلَّ* amesema, 'Ewe Muhammad (صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)! Je wewe hupo radhi na jambo hili kwamba mtu yeyote katika umma wako atakaekusalia mara moja, mimi nitamrehemu mara kumi

* Amir-e-Ahl-e-Sunnat ameitoa hotuba hii mnamo mwezi 12 Rabi'-ul-Awwal (1430 AH) katika jitimai ya maulidi ya Dawat-e-Islami (harakati ya dunia nzima ya kuitangaza Quran na Sunnah isiyo jihusisha na siasa). Imeandikwa katika maandiko pamoja na marekebisho ya lazima.

na yeyote katika umma wako atakae kusalimia mara moja, mimi nitamsalimia yeye mara kumi?’ (*Mishkat-ul-Masabih, juz. 1, uk. 189, hadithi 928*)

Mufti mwenye kutambulika Amad Yar Khan Na’imi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَظِيمِ amesema, ‘Allah عَزَّوَجَلَّ, akimsalimia mja ina maana kwamba ima anawataka Malaika wamtolee salamu yeye au wampe hifadhi kutokana na majanga na mabalaa’.

(*Mirat-ul-Manaji_, juz. 2, uk. 102*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mtumwa mweusi

Kulikuwa na msafara unaosafiri katika bara Arabu. Msafara huu ukawa umeishiwa na maji yao na wakazidiwa na kiu kali sana mpaka walikaribia kupatwa na mauti lakini walibahatika kumuona Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akito kezea mbele ya macho yao. Wote walifurahi walipomuona yeye. Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliefunuliwa mambo ya ghaibu, alietakaswa na kila aibu akasema, ‘Nyuma ya mlima ule kuna mtumwa mwenye ngozi nyeusi anapita na ngamia wake. Analo gudulia la ngozi ndani yake kuna maji. Mwambieni aje na huyo ngamia wake.’

Basi baadhi ya wale wasafiri katika msafara ule wakatoka kwenda kumuangalia na wakamuona yule mtumwa yupo juu ya ngamia wake.

Wakamleta mbele ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akali chukua lile gudulia la ngozi na akaupitisha mkono wake uliobarikiwa juu yake na akawaita, ‘Njoooni enyi wenye kiu! Ikateni kiu yenu.’ Basi wale wasafiri wote wakanywa yale maji, wakaikata kiu yao na wakajaza vyombo vyao. Baada ya kuona ule muujiza, yule mtumwa mwenye ngozi nyeusi akaubusu mkono ulio barikiwa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaupitisha mkono wake kwenye uso wa yule mtumwa.

Ile sura yake yenye ngozi nyeusi ikabadilika kabisa na ikawa nyeupe yenye kungara kama mwezi uliotimia unao angaza katika usiku wa kiza kama mchana. Akapatwa na mshangao mkubwa yule mtumwa na akaitamka shahada na akaingia katika Uislamu na moyo wake pia ukanawirika.

Alipokwenda kwa bwana wake baada ya kuwa Muislamu, bwana wake hakuweza kumtambua kama yeye ndie mtumwa wake. Yule mtumwa akasema, ‘Mimi ni mtumwa wako!’ Bwana wake akasema ‘Mtumwa wangu alikuwa mweusi.’ Mtumwa akasema, ‘Unasema kweli bwana, lakini nimesilimu

na nimekubali kumtumikia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambae ameufanya uso wangu ung'are kama mwezi uliotimia. Katika ukaribu na yeye maumivu yote yanaondoka, madhambi yote yanafutwa na kiza cha ukafiri kinaondoka kabisa na wala hakuna ajabu ya uso wangu mweusi kubadilika ukawa ni mweupe wenye kung'ara.'

(imetolewa katika tafsiri ya Mašnawi, uk. 262)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Ndugu zangu waislamu! Maisha yangu nimeyatoa muhanga kwa ajili ya Mtume aliye barikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Allah! Allah! Aliashiria kwa maelezo kamili kuwa kuna mtu mwenye ngozi nyeusi anatembea na ngamia wake nyuma ya mlima, na amebeba ngozi ya kubebea maji. Kisha kwa uwezo aliopewa na Allah عَزَّوَجَلَّ aliwanyweshwa maji wasafiri wote mpaka wakatosheka na maji yaliokuwa kwenye ngozi hayakupungua hata kidogo na isitoshe Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaupitisha mkono wake juu ya uso wa mtumwa mwenye ngozi nyeusi na akaung'arisha uso wake, bali mpaka moyo wake uling'ara na akaingia katika Uislamu.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

2. Uso wenye kung'ara

Sayyidna Asid Bin Abi Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Kuna siku moja Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliupitisha mkono wake juu ya uso wangu na kifua changu. Kwa Baraka yake nina poingia katika nyumba yoyote yenye kiza basi ile nyumba inang'ara.’ (Al-Kha_ais-ul-Kubra lis-Suyuti, juz. 2, uk. 142)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

3. Mwanga wa mwenye nuru

Ndugu wapenzi waislamu! Wakati Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anaweza kuufanya uso na kifua kung'ara kwa kuupitisha mkono wake tu, je yeye mwenyewe صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ atakuwa ana ng'ara kiasi gani? Imeelezwa katika Darimi kuwa Sayyiduna Abdullah Bin ‘Abbas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا amesema, ‘Pindi Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akizungumza, ilikuwa ikionekana kama kuna nuru inang'ara kutoka kwenye mwaya wa meno yake ya mbele.’

(Sunan Darimi, juz. 1, uk. 44, namba. 58)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

4. Kuta kung'ara

Inaelezwa katika shifaa: Kuta zilikuwa zinang'ara pindi Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anapo tabasamu. (*Ash-Shifa, uk. 61*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

5. Sindano iliyopotea

Sayyidatuna 'Aishah Siddiqah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا anasimulia, 'Siku moja katika muda wa usiku nilikuwa nyumbani nikishona nguo basi ghafla sindano ikaniponyoka mkononi mwangu na taa ya mafuta ikazimika. Katika muda huo huo Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mwenye nuru akaingia nyumbani, basi nyumba yote ikawa inang'ara kutokana na nuru ya uso wake na ile sindano iliyopotea ikaonekana.' (*Al-Qaul-ul-Badi', uk. 302*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

سُبْحَانَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ! Ni kung'ara kwa nuru kulikoje kwa Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ! Mufti mkuu mwenye kutambulika Ahmad Yar Khan عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْعَالَمِينَ amesema, 'Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni Bashar (mwanadamu) vile vile ni nuru. Ina maana yeye Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni mwanadamu mwenye nuru. Kimwili ni mwanadamu na kihakika ni Nuru.'

(*Risalah Nur ma' Rasail-e-Na'imiyah, uk. 39-40*)

Vipi kuukanusha ubinadamu wa Mtume ﷺ?

Ndugu waislamau! Bila ya shaka, uhalisia wa Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni Nuru, lakini tieni akiliini kwamba hairuhusiwi kabisa kuukanusha ubinadamu wake. Imam Ahmad Raza Khan عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ amesema, ‘Kukanusha moja kwa moja ubinadamu wa mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni kufu (kukufuru).’ (*FatawaRazawiyyah, juz. 14, uk. 358*) Lakini ubinadamu wake sio wa kawaida, yeye ni bwana wa mabwana, ni mbora na mtukufu kuliko wanadamu wote.

Quran tukufu inasema:

قَدْ جَاءَكُمْ مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُبِينٌ ﴿١٥﴾

Kwa hakika imekujieni nuru kutoka kwa Allah na kitabu chenye ubainifu.

(juz. 6, Surah Al-Maidah, aya 15)

Katika aya iliyotajwa hapo juu, nuru ina maanisha kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliebarikiwa. Sayyiduna Imam Muhammad bin Jarir Tabari (aliefariki mnamo mwako 310 H) amesema; يَعْنِي بِالنُّورِ نُحْمَدًا (صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ); maana ya Nuru (ndani ya aya) ni Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

(Tafsir-u-Iabari, juz. 4, uk. 502)

Imam Abu Bakr ‘Abdur Razzaq عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْعَمَّانِ, mwanachuoni wa hadithi anaetambulika amesimulia katika kitabu chake 'Al-Musannaf' kutoka kwa Sayyidna Jabir Bin ‘Abdullah Ansari رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا ambae amesimulia: "Nilisema, 'Ewe Rasulallah (صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)! Ninawatowa wazee wangu muhanga kwa ajili yako! Tafadhali niambie kitu gani kilicho umbwa na Allah عَزَّوَجَلَّ mwanzo kuliko vyote?' Yeye Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akanijibu, 'Ewe Jabir! Bila ya shaka, Allah عَزَّوَجَلَّ ameiumba Nuru ya Mtume wako kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kutoka katika Nuru yake kabla ya kuumba ulimwengu wote.' (Fatawa Razawiyyah, juz . 30, uk . 658)

Ndugu zangu wapenzi Waislamu! Kwa kupata maelezo zaidi kuhusu Nuru basi kajipatie faida zaidi kwa kukisoma kitabu 'Risala-e-Nur' kilichoandikwa na mufti mwenye kutambulika Ahmad Yar Khan عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

6. Alimpa kumbukumbu nzuri

Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, 'Nilisema kumwambia Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, 'Ewe Rasulallah (صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)! Mimi huwa nasikiliza kile unacho kisema lakini baadae nakisahau.' Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akanijibu, 'Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ!

Itandike kashda yako. Nikaitandika kashda yangu. Mtume wa rehema na mtetezi wa umma na wa mwanzo kuingia peponi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaweka kitu fulani kwa mkono wake wenye baraka kwenye ile kashda na akasema, 'Ewe Abu Hurah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ! Ichukue kashda yako na ikumbatie.' Nikafanya kama nilivyo agizwa. Tokea hapo (kumbukumbu yangu ikawa nzuri kiasi kwamba) sikukisahau tena kitu chochote kile alichokuwa akikisema.

(Sahih Bukhari, juz. 1, uk. 62, 94, hadith 2350)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kuwa na kawaida ya kusikiliza maongezi yanayotoa muamsho kuhusu sunna

Ndugu zangu wapenzi waislamu! Tumekuja kujua kwamba Allah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amembariki Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa kumpatia nguvu zisizo za kawaida. Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alivyokuwa na uwezo wa kumpa mtu kitu kinacho onekana vile vile alikuwa na uwezo wa kumpa kisicho onekana, kama alivyompa kumbukumbu ya ajabu swahaba wake bwana wetu Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ.

Ni wito wangu muendeleo kuwa karibu sana na mazingira mazuri ya madani ya Dawat-e-Islami, mazingira ambayo

yamekusanya upendo wa kweli kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Utayasikiliza maongezi yanayo toa uamsho katika sunna. Imani yako pia itakuwa ni yenye kuimarika sana kwa kukaa kwako na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Pendelea sana kuhudhuria katika jitimai zenye uamsho na ikiwezekana pia pendelea kusafiri na Madani Qafila (misafara ya Madani). Jisomee kila siku angalau kitabu kimoja kilicho chapishwa na Maktaba-tul-Madinah na pia sikiliza bayana katika video au katika mikanda ya kaseti. **إِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ** utapata Baraka zisizokuwa na hesabu na utapata malipo mengi ya duniani na akhera

Vipi nilijiokoa na upotofu!

Kukuraghibisha, kuna kisa cha Madani kuhusiana na Baraka zinanzopatikana katika kusikiliza kaseti na CD. Ni simulizi ya kijana mmoja kutoka Malkapur, mji katika miji ya 'Hind Baghdadi' (India); 'Niliishi nje ya nchi yangu kwa muda wa miaka mitano. Nilikaa na watu wenye imani potofu kabisa mpaka imani yangu safi ya Uislamu ilianza kuchafuka. Baadae nikarejea nyumbani India na mikanda ya kaseti 30 na video zenye imani za upotofu. Kwa Baraka za Allah **عَزَّوَجَلَّ** nikakutana na kijana mmoja Muislamu alievaa kilemba cha rangi ya kijani, alifanya 'infiradi koshish' (juhudi zake binafsi) kwa upole na huruma na akanizawadia

VCD iliyotolewa na Maktaba-tul-Madinah ya Dawat-e-Islami. Baada ya kufika nyumbani nikaangalia ile VCD¹.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ kila nilipoendelea kuiangalia huku ukungu wa imani potofu nilizokuwa nazo uliendelea kusafishika. Ile VCD ilipo maliza tu moyo wangu ukaanza kuhisi moja kwa moja kama hawa watu waliokuwa wakionekena katika ile VCD ni miongoni mwa watu wema kabisa na sura zao sio sura za waongo. Nikaweka ahadi na moyo wangu kama Sitawacha kabisa imani za watu wema kama wale niliowaona katika ile VCD. Kisha nikaziharibu zile kaseti 30 na video nilizotoka nazo kule nje ya nchi ili asije akapotea muislamu yeyote yule kwa kuziangali.’ Kwa uwezo wa Allah عَزَّوَجَلَّ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amefunuliwa mambo ya ghaibu na yeye anawafunulia wengine, basi hii hapa ni simulizi yenye mafunzo isome na ifurahie.

7. Habari ya ghaibu

Sayyidatuna Unaysah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا amesimulia: ‘Baba yangu a liniambia, ‘Nilipokuwa naumwa, Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ a likuja kunitembelea na akasema, ‘Maradhi haya hayatakusba bishia madhara yoyote yale lakini utakuwa na hali gani utak

¹ jina la hii VCD ni ‘Didar-e-Amir-e-Ahl-e-Sunnat’. Kainunue katika maduka ya Maktaba-tul-Madinah au iangalie katika mtandao moja kwa moja www.dawateislami.net.

[Majlis Maktaba-tul-Madinah]

apo pofua macho yako kwa muda mrefu baada ya mimi kuf ariki?’ Baada ya kulisikia jambo hili, nikamjibu kwa upole ka bisa, ‘Ewe Rasulallah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ! Utakapofikia wakati kama huo basi mimi nitabakia kuwa mwenye subra nikitraji a thawabu.’ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema, ‘Kama utafanya hivyo basi utaingia peponi bila ya hesabu.’ Basi baba aka pofua macho yake punde tu baada ya kufariki kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na baada ya muda fulani Allah عَزَّوَجَلَّ akamj aalia baba uoni mwengine mpaka muda wakufariki kwake.’

(Dalail-un-Nubuwwah lil-Bayhaqi, juz. 6, uk. 47)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Ndugu wapenzi waislamu! Mumeona vile ambavyo Allah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amemjaalia Mtume wetu mpendwa kwamba anafahamu ni mpaka muda gani swahaba wake ataishi hapa duniani na mambo gani yanaweza yakamfika. Aya nyingi sana za Quran zimethibitisha kujua kwake mambo ya Ghaibu. Imekuja katika aya moja katika juzuu ya 30, Surah At-Takwir, aya 24, ambapo Allah عَزَّوَجَلَّ anasema

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ﴿٢٤﴾

Na wala yeye si bakhili kwa mambo ya ghaibu

(juzuu 30, Surah At-Takwir, aya 24)

Pia kuna ushahidi ndani ya hadithi ifuatayo kwamba muislamu atakapo patwa na taklifu au moja ya matatizo au ulemavu basi anatakiwa kuwa na subra ili awe mwenye kustahiki thawabu. Sayyiduna Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: ‘Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema, “Yeyote katika waja wangu nitakae mtahini macho yake akasubiri, basi nitampa pepo badili ya macho yake.’

(Sahih Bukhari, . juzuu 4,. 6, hadithi 5653)

8. Ngamia wa ajabu

Kuna mfanya biashara mmoja siku moja alikwenda katika mji wa Makka. Abu Jahl akaenda kununua lakini akafanya udanganyifu katika malipo. Yule mfanya biashara alikasirika sana na akaenda kwa Maquraish na akasema, ‘Kuna mtu yeyote mwenye huruma na mimi akamwambie Abu Jahl anilipe?’

Wakaishiri kwa mtu aliyekuwa amekaa kitako katika kipembe kimoja msikitini na wakamuambia, ‘Kazungumze nae, bila ya shaka yeye anaweza akakusaidia.’ Wale Maqurayshi wakamuelekeza kwa ‘Yule Mtu’ ili kama atakwenda kwa Abu Jahl akamtukane na wao wangeweza kumcheka na waweze kufurahi. Basi yule mfanya biashara akamfuata yule mtu na akamsimulia mkasa wote. Akasimama na akaongozana nae mpaka kwenye nyumba ya Abu Jahl na

akabisha hodi. Abu Jahl akauliza huku akiwa bado yupo ndani nyumbani, 'Ni nani?' jawabu likatoka, 'Muhammad.' Abu Jahl akatoka, akashikwa na woga mkubwa sana. Akauliza,

'Kimekuleteni nini hapa?' Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema, 'Kwanini hujamlipa pesa yake?' Akamjibu, 'Ninamlipa sasa hivi.' Basi, akazileta zile pesa na akamkabidhi mkononi yule mfanya biashara na akarudi nyumbani kwake. Watu wakamuuliza, 'Abu Jahl ! Mbona ulikuwa na woga sana?' Akawajibu, 'Wakati Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alipotaja jina lake niliingiwa na khofu kubwa sana. Nilipotoka nilikiona kitu cha ajabu sana. Nimemuona ngamia mkubwa wa kutisha sana amesimama. Sijawahi kumuona hata siku moja maishani mwangu. Basi, nikahisi salama sana nimitii taratibu, kama si hivyo basi yule ngamia angenimeza.'

(Al-Khasais-ul-Kubra lis-Suyuti, juzuu . 1, uk . 212)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu zangu wapenzi waislamu! اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Ni mkubwa ulioje ukarimu wa Mtume wetu mpendwa, Mtume wa ulimwengu wote, tulizo la moyo, mkarimu na mwenye huruma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Namna gani alivyokuwa akiwasaidia wenye shida na matatizo na akiwasimamia waliodhulumiwa mpaka kupatiwa haki zao. Na pia Allah

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ nae ni mkarimu sana kwa Mtume kama anavyo mpatia ushindi dhidi ya maadui zake!

Kwa upande mwengine, Abu Jahl alieandikiwa kukosa fadhila za imani, akabaki vilevile na ukafiri wake licha ya ku ushuhudia muujiza kama ule kwa macho yake.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

9. Simba wamefika

Isikilizeni simulizi hii yenye mafundisho ndani yake inayoelezea muujiza mwengine wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na upofu wa ndani kabisa wa Abu Jahl. Kwa kuwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa akiwalingania watu kwenye uongofu, makafiri wa Quraishi wakaanza kuwa maadui zake na wakimuudhi yeye kwa njia tofauti tofauti. Kuna siku Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa anapita katika bonde liitwalo hajun

Mmoja katika maadui aitwae 'Nadhr' akajitokeza mbele yake kutaka kumuua. Alipomkaribia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Nadhr akaanza kutetemeka na akakimbia kwa hofu kurudi mjini. Abu Jahl, baada ya kuona mkasa wote akamuulizia kilichomfanya awe vile. Akamjibu, 'Leo nilimfuata Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ili nimuue. Nilipomkaribia

nikawaona simba wengi wananinjia na wamefungua vinywa vyao wananguruma nawana saga saga meno yao, basi pakawa hapana njia yoyote isipokuwa kukimbia.’ Licha ya kuusikiliza muujiza huo, Abu Jahl akasema, ‘Hizo ni katika njama za uchawi za Muhammad.’ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ (Allah عَزَّوَجَلَّ aepushe). (*Al-Khasais-ul-Kubra lis-Suyuti, juz. 1, uk. 215*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

10. Wazazi wamefufuka

Kila mmoja anawapenda wazazi wake basi kwa nini Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ asiwe na upendo huo kwa wazee wake! Kutokana na uwezo na nguvu alizopewa na Allah عَزَّوَجَلَّ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alifanya muujiza mmoja mkubwa sana ili awafanye wazazi wake kuwa katika umma wake. Basi soma kisa cha muujiza kifuatacho na ufurahi. Imam Abul Qasim ‘Abdur Rahman Suhayli (aliefariki mwaka 581AH) amenukuu ndani ya ‘Ar-Raudh-ul-Unuf kwamba Umm-ul-Mu’minin Sayyidatina ‘Aishah Siddiqah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا anasimulia kwamba Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliomba dua, ‘Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Wahuishe wazeee wangu.’ Allah عَزَّوَجَلَّ akaijibu Du’a ya Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akawafufua wazee wake kutoka makaburini. Wote wawili wakamuamini Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآLِهِ وَسَلَّمَ na wakarejea makaribuni mwao.’ (*Ar-Raud-ul-Unuf, juz. 1, uk. 299*)

Wazazi wake walimpwekesha Allah ﷺ

Pindi Mtume ﷺ alipokuwa ndani ya tumbo lenye Baraka la mama yake Sayyidatuna Aminah رضى الله تعالى عنها, baba yake Sayyiduna ‘Abdullah رضى الله تعالى عنه alikuwa tayari ameshafariki dunia. Na wakati Mtume ﷺ anatimia umri wa miaka 5 au 6, mama yake رضى الله تعالى عنها pia naye akafariki dunia. Mtume ﷺ akautangaza utume wakati ana umri wa miaka 40. Kwa hiyo hapa asifikiri mtu kwamba wazazi wake Mtume ﷺ wamefariki dunia katika hali ya ukafiri na wakapatiwa adhabu katika makaburi yao, ndio maana Mtume mtukufu ﷺ akawasilimisha na kuwatamkisha shahada ili awasilimisha kutokana na adhabu ya kaburi. La si hivyo bali kiuhalisia katika maisha yao hawakuwahi kabisa kuabudia masanamu na walikuwa ni miongoni mwa wanao mpwekesha Allah ﷺ. Mtume ﷺ akawafufua kwa uwezo wake Allah ﷻ na wakaitamka shahada ili wawe miongoni mwa umma wake.

Samaki aliemmeza Nabii Yunus عليه السلام ni samaki wa peponi

Sayyidna Ismail Haqqi عليه رحمة الله القوي amenukuu katika Tafsir Ruh-ul-Bayan, ‘Mtume Yunus عليه السلام alibakia katika tumbo la samaki kwa siku tatu, siku saba au siku

arubaini; kwa hiyo samaki huyu ataingia peponi.’ (*Ruh-ul-Bayan, Juz.5, uk. 226, 518*)

Wazazi waheshimiwa wataingia peponi

Ndugu Waislamu! Tafakarini tu! Samaki ambaye aliishi nda ni ya tumbo lake siku chache Mtume wa Allah ﷺ Sayyidna a Yunus عَلَيْهِ السَّلَام ataingia peponi, itawezekana vipi kwamba Bibi Aminah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا afariki hali ya kuwa ni kafiri na aingie kaburini akaadhibiwe, wakati Bwana wa Sayyidna Yunus صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Mtume Muhammad Mustafa عَلَيْهِ السَّلَام alibebwa katika tumbo lake kwa miezi kadhaa. Bila shaka wazazi wake wawili رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا walitumia uhai wao katika kumpwekesha Allah ﷻ na ni miongoni mwa watu wa peponi. Aidha, mababu wote wa Mtume wetu mpendwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ walikuwa ni miongoni mwa watu wema. Kwa maelezo zaidi kuhusu hilo tafadhali kajisomee Fataawa Razawiyyah, juzuu ya 30, kutoka ukurasa 267 mpaka 305.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

11. Mbuzi aliekufa alihuika

Sayyidna Jabir Bin Abdullah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ mara moja alikuja kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaona athari ya njaa katika uso wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Muda huo huo akarudi nyumbani

kwake na akamuuliza mke wake, ‘Kuna chakula chochote nyumbani?’ Akajibu, ‘Hamna chochote zaidi ya mbuzi huyu na unga kidogo tu.’ Yeye mara moja akamchinja yule mbuzi na kumuamuru mke wake aipike nyama yake na mkate. Sayyiduna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ anasema, ‘Chakula kilipokuwa tayari, nikakipeleka kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Mtume wa Rahmah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema, ‘Ewe Jabir, nenda kawaite watu.’ Nikatekeleza nilicho agizwa. Masahaba عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ walipofika, Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akatoa agizo, ‘Walete kwangu katika makundi madogo madogo.’ Wakawa wanaingia kidogo kidogo, wanakula chakula na wanaondoka. Wote walipomaliza kula nikaona chakula kiko vile vile hakijapungua hata kidogo kwenye chombo. Mtume mtukufu aliwaagiza watu kwamba wale nyama ya yule mbuzi lakini wasivunje mifupa yake.

Basi Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaikusanya ile mifupa ya yule mbuzi akaweka mkono wake wenye baraka na akasoma kidoga. Muda si mrefu yule mbuzi ambae ililiwa nyama yake akawa amesimama mbele yetu anatikisa masikio yake. Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema, ‘Ewe Jabir! chukua mbuzi wako.’ Niliporejea nyumbani na yule mbuzi, mke wangu akaniuliza, ‘Mbuzi huyu umemtoa wapi?’ Nikamjibu, ‘Wallahi! Huyu ni mbuzi yule yule tuliemchinja. Allah عَزَّ وَجَلَّ amemuhuisha tena kwa dua ya Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

(Al-Kha? Ai? -ul-Kubra, juz. uk112)

12. Mtoto anafufuka

Mpenzi mkubwa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ‘Allamah ‘Abdur Rahman Jami كَاتِبُ التَّوْرَانِي أَنَسِمْ anasimulia, ‘Sayyidna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alimchinja mbuzi mbele ya wanawe. Alipoondoka baada ya kumaliza, watoto wakachukua kisu na wakapanda juu ya dari la nyumba na mkubwa akamwambia mdogo wake, ‘Njoo! mimi nitakufanyia kama baba alivyo mfanyia mbuzi.’ Kaka mkubwa akaifunga mikono ya yule mdogo wake, akakipitisha kisu kwenye shingo yake na akamkata kichwa chake na akakibeba mkononi mwake. Mama yao alipoona akaja mbio na yule mtoto mkubwa nae akaanza kukimbia kwa hofu. Hatma yake akaanguka kutoka katika dari na akapoteza maisha. Mama aliekuwa mwenye subira licha ya kuwapoteza watoto wake wote wawili hakupiga mayowe na makelele kwasababu hakutaka kumsumbua mgeni wake mtukufu ambae ni rehema kwa walimwengu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Kwa uvumilivu na subira ya hali ya juu kabisa akaileta miili ya watoto wake ndani ya nyumba na akaifunika kwa kitambaa na hakumwambia yeyote hata mume wake Sayyiduna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ. Ingawa moyo wake ukawa unamwaga machozi ya damu, lakini aliendelea kutabasamu na kuonyesha furaha usoni mwake na akaendelea kuandaa

chakula. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akawasili na chakula kikawa tayari. Katika muda huo huo, malaika Jibril عَلَيْهِ السَّلَام akaja na akasema, ‘Ewe Rasulallah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ! Allah عَزَّوَجَلَّ anakuamrisha umwambie Jabir awalete watoto wake ili wapate bahati ya kula chakula pamoja na wewe. Mtume رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ akamuagiza sayyidna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ awalete watoto wake. Hapo hapo akaenda kumuuliza mke wake, ‘Watoto wako wapi?’ Mke wake akamuomba amuarifu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwamba watoto hawapo.

Rasulullah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasisitiza sana watoto waletwe kama Allah عَزَّوَجَلَّ alivyoamrisha. Mke wake Sayyiduna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alianza kulia na akamwambia, ‘Siwezi kabisa kuwaleta watoto.’ Sayyidna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ akauliza, ‘Kumetokezea nini, mbona unalia?’ Akaja nae mpaka ndani na akampa khabari ya msiba uliowafika na akafunua kile kitambaa alichofunikia wale maiti. Baada ya kuona hali hii, Sayyiduna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ nae pia akaanza kulia. Kisha Sayyidna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ akaichukua ile miili mpaka mbele ya Mtume wa rahma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Sauti za vilio zika anza kusikika kutoka katika ile nyumba.

Allah عَزَّوَجَلَّ akamtuma malaika Jibril عَلَيْهِ السَّلَام akimwambia, ‘Ewe Jibril! Mpe khabari Mtume wangu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwamba mola wake anasema; ‘Ewe Mtume wangu

mpendwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ wewe omba dua na mimi nitawafufua.’ Basi Mtume wa walimwengu, tulizo la akili na moyo wetu, mkarimu na mwenye huruma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaomba dua na watoto wote wawili wakafufuka kwa amri yake Allah عَزَّوَجَلَّ. (*Shawahid-un-Nubuwwah, uk. 105; Madarij-un-Nubuwwah, juz. 1, uk. 199*)

Allah عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe madhambi yetu kwa baraka yao!

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu zangu wapenzi waislamu! Mumeona utukufu wa Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ! Chakula kidogo kiliwatosha watu wengi na hakikupungua. Kama haitoshi akasoma juu ya mifupa ya mbuzi na mbuzi yule akasimama akitikisa tikisa masikio yake. Vile vile akawafufua watoto wa Sayyidna Jabir رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ kwa amri yake Allah عَزَّوَجَلَّ.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Aliemtusi mtume ametupwa nje ya kaburi

Ndugu wapenzi waislamu! Sasa someni kisa chenye mazingatio cha mtu mbaya aliekanusha utukufu wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Pia utapata kujua namna gani Allah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anavyo walipizia kisasi maadui wa kipenzi chake Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Sayyiduna Anas صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, 'Kuna mkristo mmoja alisilimu na akajifunza suratul baqarat na suratul imran na akawa muandishi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Baadae akaritadi na akarejea katika ukristo. Alikuwa akisema; مَا يَدْرِي مُحَمَّدٌ إِلَّا مَا كَتَبْتُ لَهُ; yaani 'Muhammad hajui chochote isipokuwa kile nilichom uandikia mimi.' Basi baada ya siku chache tu Allah عَزَّوَجَلَّ akaivunja shingo yake, ina maana alikufa kifo kisicho kawaida.

Wenzake wakaenda kuchimba kaburi na kumzika. Asubuhi kaburi likamtupa nje. Walipoona (mwili wake umetolewa nje) wakasema Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na wenzake ndio waliofanya haya kwa sababu aliwakimbia. Wakachimba kaburi la chini zaidi na wakamzika ndani yake lakini asubuhi ya pili kaburi lilimtupa nje kwa mara nyengine. Wakasema tena kwamba Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na wenzake ndio waliofanya jambo hili. Kwa mara ya tatu, wakalichimba kaburi lenye kina kirefu zaidi kwa mwisho wa uwezo wao na wakamzika. Asubuhi ya tatu kaburi likamtupa nje. Hapo sasa wakatambua kwamba jambo hili halikufanyiwa na binadamu. Mwisho wakaamua kuuwacha mwili wake nje bila ya kuzika. (*Sahih Bukhari, juz. 2, uk. 506, hadithi 3617*)

Kukanusha elimu ya mtume kumesababisha kifo kibaya

Ndugu waislamu! Je, mumeona! Yule mtu hakuuthamini utukufu wa kuwa pamoja na kiumbe bora kuliko wote hapa duniani. Akaritadi na akapinga elimu ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Hatimae akafa kifo kibaya sana mpaka ardhi ikakataa kumpokea kabisa. Jambo hili linaonesha kwamba kukanusha elimu ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kunachangia sana mtu kupoteza dira hapa hapa duniani na kesho akhera vile vile. Muislamu hawezi kabisa kukanusha elimu ya Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, ni wanafiki peke yao ndio watakao kanusha. Kuna mtu mmoja amesema ‘الْتِفَاقُ يُورِثُ الْإِعْتِرَاضَ’ unafiki unarithisha ukanushaji.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Ndugu waislamu! Mwisho wa maongezi yangu, ningependa kuchukua nafasi hii kuwatajia baadhi ya sunna na adabu. Mtume wa rahma, wa mwanzo kuingia peponi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Yeyote anaependa sunna yangu basi amenipenda mimi na anaenipenda mimi atakuwa na mimi peponi.’

(Mishkat-ul-Masabih, juz. 1, uk 55, hadithi 175)

Lulu za madani 14 kuhusu kupeana mikono

- ❖ Ni Sunna kwa waislamu wawili wanaposalimiana kupeana mikono.
- ❖ Wakati wa kuaga ni sunna kuna kutoa salamu na kupeana mikono pia kumeruhusiwa.
- ❖ Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema kuwa waislamu wawili wanapo salimiana na wakaulizana hali zao basi Allah عَزَّوَجَلَّ huwatumia rehma mia moja baina yao. Rehma tisiini humshukia yule aliesalimia kwa bashasha zaidi kuliko mwengine na akaulizia hali ya mwenzake. *(AL Mu'jam-ul-AWSAt, Juz. 5, uk 380., hadith 7672)*
- ❖ Marafiki wawili wanaposalimiana na kupeana mikono na wakamslia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ basi madhambi yao yalopita na yajayo yatafutwa kabla ya hata hawajaachana *(Shu'ab-ul-Iman lil-Bayhaqi, Juz. 6, uk. 471, hadithi 8944)*
- ❖ Wakati muna salimiana mumsalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na ikiwezekana musome dua hii pia يَغْفِرُ اللهُ لَنَا وَلَكُمْ (Allah عَزَّوَجَلَّ anisamehe mimi na wewe.)
- ❖ Dua watakayo omba waislamu wawili wakati wakupeana mikono itajibiwa إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ na watasamehewa kabla mikono yao haijaachana إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ. *(Musnad Imamu Ahmad Bin hanbal, Juz. 4, uk. 286,! hadithi 12454)*

- ❖ Kupeana mikono huondoa uadui.
- ❖ Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema, ‘Muislamu yeyote anaemsalimia mwenzake kwa kumpa mkono na pakawa hakuna hata mmoja anahisi uadui na mwenzake, Allah عَزَّوَجَلَّ atawasamehe madhambi yao wote wawili kabla ya mikono yao kuachana na yeyote anaemuangalia muislamu mwenzake kwa upendo na akawa hana uadui basi madhambi yao yaliopita yatafutwa kabla ya macho yao hayajaachana. (*Kanz-ul-'Ummal, Juz. 9, uk. 57*)
- ❖ Mtu anaweza kupeana mikono na mwenzake kila wakikutana
- ❖ Sio Sunna kupeana mikono kwa mkono mmoja. Sunna ni kwa mikono miwili.
- ❖ Baadhi ya watu hupeana mikono kwa kupeana vidole tu; jambo hili si katika Sunna.
- ❖ Ni makuruhu mtu kubusu mkono wake mwenyewe. Walio na tabia ya kubusu mikono yao wenyewe baada ya kupeana mikono wajaribu kuepuka tabia hiyo. (*Bahar-e-Shari'at, Juz. 16, uk. 115Mulakhkhasan*)
- ❖ Kama kupeana mikono na Amrad (mwanamume anaevutia) kunasababisha matamano basi hairuhusiwi kupeana nae mikono. Bali ikiwa kuangaliana nako

kunasababisha matamaniao basi kumunagalia pia ni dhambi. (*Durr-e-Mukhtar, Juz. 6, uk. 98*)

- ❖ Utaratibu wa sunna katika kupeana mikono ni kuwa kusiwepo na kizuwizi kama vile kitambaa n.k baina yenu bali kila kiganja kinatakiwa kigusane na kiganja chengine. (*Bahar-e-Shari'at, Juz. 16, uk. 98*)

Ili kujifunza maelfu ya sunna, kanunue vitabu viwili vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madina, 'Bahar-e-Shari'at', Sehemu ya 16 (kurasa 312) na 'Sunnatayn aur Adab' (kurasa120). Njia moja bora kwa ajili ya kujifunza sunna ni kusafiri katika misafara ya Madani na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Kumuona Mtume Mtukufu ﷺ

Baada ya kumalizika ijtimai ya kimataifa (inayofanyika katika mji wa Multan) ya siku tatu ya Dawat-e-Islami (harakati ya ulimwengni isiyo jihusisha na siasa, ya kuitangaza Quran na sunna) Madani Qafla (misafara) ya wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ wanasafari kuelekea katika vijiji na miji kwa ajili ya kuifundisha sunna. Baada ya jitimai iliyofanyika katika mwaka 1426, Madani Qafla moja iliotoka katika eneo la Agra Taj (Bab-ul-Madinah, Karachi) walisafiri kuelekea baadhi ya maeneo na wakafikia msikitini

kama utaratibu ulivyo katika Madani Qafla. Usiku watu walipolala, ndugu muislamu mmoja alipata bahati ya kumuona Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwenye ndoto akiwa ana furaha sana. Akabainaikiwa kama dawat-e-Islami ni harakati ya watu wema wanaoitangaza sunna na akawa amejitolea katika mazingira ya madani kimwili na kiroho.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu zangu wapenzi waislamu! Mumeona! Kwa baraka ya kuwa na pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ yule ndugu muislamu alipata bahati ya kumuona Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika ndoto. Bila shaka suhuba ya wapenzi ina faida nyingi mno. Soma faida nyingine iliopatikana kwa baraka ya kusuhubiana na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na utafurahi.

Nilikuwa mpenzi wa filam za kigeni

Ndugu mmoja wa Kiislamu kutoka jeshini amesema: 'Nilikuwa ninaongoza katika maisha ya dhambi na nilikuwa na kaseti mia moja za nyimbo. Nyimbo nyingi zilikuwa ni zenye maneno ya kukufuru مَعَادَ اللهِ عَزَّوَجَلَّ. Kuangalia filamu za kigeni ilikuwa ni jambo ninalolipenda zaidi. Kusikiliza nyimbo, vichekesho, kucheza karata, n.k. ilikuwa ni katika ratiba yangu ya kila siku. Nilikuwa ni mtu nisiejali kabisa na

nilikuwa mkorofi sana kwa wazazi wangu. Kulikuwa hakuna tabia mbaya nilokuwa mimi sinayo. Baadae nikajiunga na jeshi na nikahama kutoka Rawalpindi kwenda Quetta. Wakati nipo njiani, nikawa ninawakera wasafiri wote katika treni. Nilipofika tu pale **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ** nikakutana na kijana mmoja wa Dawat-e-islami. Alikuwa amevaa kilemba cha rangi ya kijani na alikuwa amehusiana na Gulzar-e-Taybah (Sargodha).

Akanifanyia juhudi binafsi na akaanza kunichukua kwenda katika jitimai za kushajiisha sunna ya kila wiki. Akaniathiri kwa tabia zake njema na nasaha zake maneno yake matamu. Nikatubia madhambi yangu yote yaliyopita nyuma na nikajilazimisha kukaa karibu ya mazingira ya madani, **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ** zaidi nikapata shauku ya kusafiri pamoja na wafuasi wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** kwa muda wa masiku 30. Na sasa hivi niko kama msimamizi wa sehemu katika kitengo kimoja wapo nikifanya juhudi ya kuwashawishi wengine kuzifanyia kazi sunna na kusimamimisha sala **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ**.

Upendo kwa wacha mungu kunaleta thawabu ikiwa...

Ndugu waislamu! Mumeona! Kuwa pamoja na wafuasi wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** na kuwa na upendo kwa wacha

mungu kumemletea mtu muovu mabadiliko katika maisha yake. Hivyo basi na wewe pia jitahidi kuwa na upendo nao. Wanaosafiri katika misfara ya madani wanabahatika kupata mambo haya mawili (suhuba ya watu wema na mapenzi kwao). Upendo kwa wacha mungu ni jambo lenye kheri kubwa mno lakini upendo huu sharti uwe ni kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Mapenzi yanayotokana na baadhi ya maslahi ya mambo ya kidunia au maslahi ya kifedha au kwa ajili ya kujipendekeza, maongezi, mali, uzuri na madaha hayo huwa si mapenzi kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Hata mapenzi kwa wazazi, watoto, au hata baadhi ya jamaa kwa undugu wa kidamu, hakuleti thawabu mpaka mtu awe ana nia ya kumridhisha Allah **عَزَّوَجَلَّ**.

Mufti mwenye kufahamika Mufti Ahmad Yar Khan **عَلَيْهِ رَحْمَةُ** **عَزَّوَجَلَّ** amesema akieleza ‘mapenzi kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**: ‘Mtu ampende mwenzake kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** na wala si kwa maslahi yoyote ya kidunia na mapenzi hayo yasiwe ajili ya majivuno. Inajumuisha mapenzi ya wazazi, watoto, jamaa na waislamu wote ikizingatiwa mtu awapende kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Mapenzi ya wacha mungu **رَحْمَتُهُمُ اللَّهُ تَعَالَى** na mitume **سُبْحَانَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ، عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ** ni kiwango cha juu sana katika kumpenda kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Tunamuomba Allah **عَزَّوَجَلَّ** atubariki kwa mapenzi hayo’. (*Mirat, juz. 6, uk. 584*)

Fadhila 8 za kupenda kwa ajili Ya Allah ﷺ

- ❖ Allah ﷺ atasema katika siku ya Qiyama, ‘Wako wapi wale waliopendana kwa ajili ya utukufu wangu? Leo nitawaweka chini ya kivuli changu. Leo hakuna kivuli ispokuwa kivuli changu.’ (*Muslim, uk. 1388, hadithi 2566*)
- ❖ Allah ﷺ anasema, ‘Mapenzi yangu yatakuwa ni wajibu (lazima) kwa wale wote wanaopendana wao kwa wao kwa ajili yangu na wakakaa kwa ajili yangu na wakakutana kwa ajili yangu na wakatumia pesa zao kwa kwa ajili yangu.’ (*Al-Muwata, juzl. 2, uk. 439, hadith 1828*)
- ❖ Allah ﷺ amesema, ‘Wale wote wanaopendana wao kwa wao kwa ajili ya utukufu wangu kutakuwa na mimbari ya nuru kwa ajili yao. Mitume na mashahidi watawaangalia wao kwa pendo.’ (*Tirmizi, juz. 4, uk. 174, hadithi 2397*)
- ❖ Ikiwa watu wawili watapendana wao kwa wao kwa ajili ya Allah ﷺ na mmoja akawa yupo kaskazini mwa dunia na mwengine akawa yupo mashariki basi Allah ﷺ atawaleta siku ya hukumu wote wawili na atasema ‘Huyu ndie uliyempenda kwa ajili yangu.’ (*Shu’ab-ul-Iman, juz. 6, uk. 492, hadith 9022*)
- ❖ Peponi kuna nguzo za Yaqut(vito vyekundu) ambazo

zina vyumba juu yake vilivyo tengenezwa kwa zumaridi (mapambo ya thamani) na milango yake ipo wazi. Vyumba hivi vinang'ara kama zinavyo ng'ara nyota. Watu wakauliza, 'Ewe Rasulallah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni nani atakaekuja kuishi humo? Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu, 'Wale waliopendana kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ, walikutana na wakakaa pamoja.' (*Shu'ab-ul-Iman, juz. 6, uk. 487, hadith 9022*)

- ❖ Wale wanaopendana kwa ajili ya Allah watakuwa juu ya viti vilivyo tengezewa kwa Yaqut (vito vyekundu) pembezoni mwa Arsh. (*Al-Mu'jam-ul-Kabir, juz. 4, uk. 150, hadith 3973*)
- ❖ Yeyote anapenda kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ, na akachukia kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ akatoa kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ na akazuia kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ basi ameiweka sawa kabisa imani yake. (*Abu Dawud, juz. 4, uk. 290, hadithi 4681*)
- ❖ Ikiwa watu wawili watapendana kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ basi watatengana ikiwa mmoja wao atatenda dhambi. Hii ni katika dalili za mapenzi kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ Kama kuna yeyote atakae tenda dhambi basi mwengine awe mbali nae.

(Kupata maelezo zaidi, soma Bahar-e-Shari'at juzuu ya 16, ukurasa wa 217 mpaka 222 kilicho chapwa na Maktaba-tul-Madinah)

Kuandika **ص** badili ya sala ya Mtume ni haramu

Sadr-ush-Shariah, Badr-ut-ariqah, ‘Allamah Mufti Muhammad Amjad ‘Ali Azami رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِيّ amesema, 'Ni faradhi (kwa muislamu) kumsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja katika maisha yake. Katika mkusanyiko, ni wajibu kumsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ muda wowote atakapotaja jina lake au kulisikia kutoka kwa mtu mwingine. Hata kama mtu atalisikia jina la Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ likitajwa mara mia moja katika mkusanyiko mmoja basi anatakiwa amsalie Mtume kwa kila mara atakayosikia. Atakaelisikia jina lenye Baraka na akawa hajamsalia basi anatakiwa amsalie hata baadae. Mtu atakaeandika jina lenye Baraka la Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa mujibu wa baadhi ya wanazuoni, ni wajibu kuiandika sala ya mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ pamoja na jina lake. Siku hizi watu wengi wanaifupisha sala ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na wanaandkika, ص, عم, صلعم, ص, عم, ص, عم au (SAW) au (PBUH). Jambo hilo haliruhusiwi na ni haramu. Vile vile baadhi ya watu huwa wana andika رَض na رَض badala ya kuandika رَضِي اللهُ تَعَالَى عَنْهُ na رَضِي اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ Jambo hili pia halitakiwi'

(Bahar-e-Shari'at, juz 3, uk. 101-102)

Unapoandika jina tukufu la Allah عَزَّوَجَلَّ basi uandike عَزَّوَجَلَّ au جَلَّ جَلَالُهُ kwa ukamilifu.

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Baraka Za Sunnah

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilohusisha na siasa) sunna za Bwana Mtume ﷺ zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah ﷻ pamoja na nia zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoshi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume ﷺ katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thababu na kujifunza sunna za Bwana Mtume ﷺ. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo **بِسْمِ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ** tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume ﷺ na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" **بِسْمِ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ**

Kwa ajili ya kusuluhisha nafsi yangu nita fuata Madani In'amaat na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafilah. **بِسْمِ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ**



www.dawateislami.net



MC 1266

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262

Web: www.dawateislami.net | E-mail: translation@dawateislami.net